**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

**Tovuti:** www.hlpc.go.tz
**Simu:** 0750059900 **Barua Pepe:**hlpc@afya.go.tz

# TANGAZO

## MATOKEO YA MTIHANI WA USAJILI ULIOFANYIKA OKTOBA 2025

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu watahiniwa wote waliofanya mtihani wa usajili mwezi Oktoba 2025 kuwa Matokeo yametoka. Kila mtahiniwa atapata matokeo kwenye akaunti yake ya mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***. Wote waliofaulu mtihani wa usajili wanahimizwa kufanya maombi ya usajili wa kudumu.

Aidha, Wahitimu wa kada ya maabara wanasisitizwa kuomba usajili wa awali kabla ya dirisha kufungwa tarehe 30.01.2026

1. Mwombaji wa usajili lazima ambaatanishe nyaraka zifuatazo ili maombi yake yafanyiwe kazi kwa wakati.
   - Cheti cha kuzaliwa
   - Cheti cha elimu ya sekondari
   - Cheti cha matokeo ya chuo (Transcript)
   - Cheti cha taaluma cha chuo (Kwa waombaji wa usajili wa kudumu)
   - Cheti cha utambuzi kutoka TCU (Kwa wahitimu waliosoma vyuo vya nje ya nchi)
2. Maombi haya yanafanyika kwenye mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***. Waombaji wote wanasistizwa kutunza jina tambuzi (username/email) pamoja na nywila (password) zilizotumika wakati wa kufungua akaunti kwenye mfumo wa HPRS muda wote kwani akaunti hiyo itatumika kwa kipindi chote.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na:
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
02.12.2025